# MTIHANI WA DARASA LA SABA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA

# KISWAHILI

***Soma vifungu vifuatavyo, vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila pengo umepewa majibu manne. Chagua jawabu lifaalo zaidi.***

Katika __1__ yetu ya Kenya, ukulima ndio __2__ wa mgongo wa uchumi wetu. __3__ wa mvua __4__, shughuli za utayarishaji mashamba na upanzi hushika __5__. Baada ya mimea kuota, na kuchipuka, wakulima huipalilia ili kuondoa __6__. Muda si muda mimea unawiri. Inapostawi mkulima huya __7__ matawi ili ipate uzao mwafaka. Ni jambo __8__ mkulima kujitayarisha kwa __9__ za kutosha akwa mfano mbolea, dawa na kadhalika.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. taifa | B. inchi | C. kaunti | D. nchi |
| 2. | A. mfupa | B. uti | C. uchi | D. shina |
| 3. | A. msimu | B. wakati | C. majira | D. upinde |
| 4. | A. unapokaribia | B. inapokaribia | C. inapokuja | D.unapokaribia |
| 5. | A. joto | B. moto | C. moshi | D. tama |
| 6. | A. matongo | B. mabaka | C. magugu | D. matawi |
| 7. | A. kata | B. chuna | C. chuma | D. pogoa |
| 8. | A. aula | B. njema | C. nzuri | D. dhaifu |
| 9. | A. bidhaa | B. shughuli | C. pembejo | D. vyombo |

Sipendi jinsi __10__ hisia __11__ kikabila zimekuwa __12__ miongoni mwetu. Ikumbukwe vyema kuwa __13__, sharti tutangamane vyema katika shughuli zetu zote kila siku. __14__ ukabila na kutupilia mbali mawazo __15__ yasiyo na manufaa kwetu Wakenya.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A. vile | B. ambavyo | C. ambazo | D. ambayo |
| 11. | A. ya | B.wa | C. za | D. la |
| 12. | A. zikijikita | B. zinajikita | C. zimejikita | D. zajikita |
| 13. | A. damu ni damu si kitarasa | | B. udugu ni kufaana si kufanana | |
| | C.umoja ni upendo | | D. vita vya panzi furaha ya mvuvi | |
| 14. | A. tuangamize | B. tudumishe | C. tusidunishe | D. tukuze |
| 15. | A. bora | B. chanya | C. duni | D. thabiti |

**Jibu kulingana na maagizo.**

16. Chagua kundi lenye nomino za wingi pekee.

A. Mafuta, mate, machozi

B. Tita, jopo, pakacha

C. Mwekahazina, mkazahau, mlariba

D. Upendo, upole, wema

17. Jibu salamu "Nashikamoo" hujibiwaje?

A. marahaba

B. shikamoo

C. kuzinawe

D. starehe

18. ***Chagua kielezi katika sentensi hii***

Maji ya mvua yamejaa tele mtunguni.

A. maji, mvua

B. tele, mtungini

C. yamejaa, tele

D. ya, tele

19. Ni methali gani inayoafikiana na maelezo haya; "haifai kuwadharau watu waliokusaidia hapo awali huenda ukawahitaji baadaye.

A. Koti la babu halikosi chawa

B. Kizuri chako kibaya cha mwingine

C. Mpanda ngazi hushuka

D. Usitukane wakunga na uzazi ungalipo

20. Ndugu mdogo wa mtu ni

A. mnuna

B. mlungizi

C. mziwanda

D. chudere

21. Mpelelezi wa siri ndani ya nchi au nchi nyingine huitwa;

A. mamluki

B. jasusi

C. kibaraka

D. mpekuzi

22. Ni sentensi ipi iliyotumia kwa kuonyesha pamoja na;

A. tatu kwa sufuri

B. aliendа kwao moja kwa moja

C. sherehe hiyo ilihudhuriwa na wazee kwa vijana

D. timu ya Arsenali iliwafunga Chelsea mabao mawili kwa nunge.

23. ***Andika kwa wingi***

Anaipenda nyama ya nyani kuliko ya bata.

A. Tunazipenda nyama za nyani kuliko za bata.

B. Wanazipenda nyama za manyani kuliko za mabata.

C. Wanaipenda nyama ya manyani kuliko za mabata.

D. Unazipenda nyama za nyani kuliko za mabata.

24. ***Maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo ni***

Kama unataka <u>kufaulu</u> soma <u>kwa baidii</u>.

A. kitenzi , kivumizi

B. kiwakilishi, kitensi

C. kielezi, nomino

D. kitenzi, kielezi

25. Buda ni kwa ajuza, _______ ni kwa ghulamu.

A. kapera

B. banati

C. bin

D. mseja

26. Rangi ya masizi ni

A. nyeusi

B. nyeupe

C. bitimarembo

D. nyekundu

27. ***Tumia kiunganishi kifuatacho***

Bakari alihudhuria kongamano kuchoka_____ kuchoka.

A. kwa minajili ya

B. madhali

C. bighairi ya

D. zaidi ya

28. ***Kanusha;***

Harmonise huimba vyema.

A. Harmonise haimbi vyema.

B. Harmonise hataimba vyema.

C. Harmonise hakuimba vyema.

D. Harmonise huwa haimbi vyema.

29. Shairi lililo na mishororo mitano katika kila ubeti huitwa;

A. tathnia

B. takhmisa

C. tathlitha

D. tarbia

30. Nomino hizi upatikana katika ngeli gani

Msikitini, sokoni, sebuleni, darasani

A. PAKUMU

B. U-I

C. I-ZI

D. LI-YA

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 – 40.**

Watoto wa kati ya miaka aruba hadi hamsa hupelekwa katika shule za chekechea ili kuanza maisha ya shule ambayo huchukua tarkibani miaka mitatu pale.

Ingawa tunafahamu fika kuwa mwalimu wa kwanza ni mzazi au mlezi, elimu hiyo ya nyumbani huwa haizingatii mtaala(silabasi) wowote ule. Hivyo basi masomo asili huanza wakati wa chekechea anapopelekwa shuleni na kusajiliwa. Shule hii ya awali katika maisha ya mwanafunzi ni muhimu kiasi cha haja. Mbali na masomo maalum, walimu huendeleza malezi pamoja na makuzi ya wana wanaokabidhiwa mikononi pao na wazazi wa watoto hawa.

Ili waweze kuwasiliana na wanafunzi hawa wadogo, sharti pawe angalau lugha moja wanayoelewa au kuijua. Katika sehemu za mashambani ambako wengi wa wakazi huwa na lugha moja ya asili au ya mama, chekechea hunafasika pakuwa kufunzwa na kuitumia shuleni.

Mbali na hayo, mijini hakuna lugha moja ya asili au ya mama kwani kuna jamii nyingi tofauti. Aghalabu shule hutwikwa jukumu la kuteua kati ya lugha ya kuwasiliana baina ya Kiingereza na Kiswahili, lugha hiyo teule hupewa nafasi ya kwanza. Hii inamaanisha kuwa hakuna mfumo rasmi au mitaala ya kielimu inayoshughulikia wana hawa wadogo.

Ni jambo ambalo linastahili kuangaziwa nchini na wadau husika. Ikumbukwe kuwa katika sehemu za mijini kuna watu wa matabaka mbalimbali. Wapo matajiri wakubwa zaidi na vilevile maskini hohehahe.

Hapa pana maana kuwa shuleni wanakowapekeka watoto wao mifumo pia ni tofauti . Shuleni za mabwebyebye husisitiza zaidi matumizi ya lugha ya ung'eng'e pengine kufuata maagizo au mapenzi ya wazazi wao. Vivyo hivyo katika shule za kibinafsi, kiingereza huweza kutumiwa zaidi.

Kwa upande mwingine shule nyingi za umma, lugha zote mbili hutumiwa matumizi ya Kiswahili sanifu yakianza mapema shuleni pia yatachangia kupigia vita lugha simo ya "Sheng' ambayo inakita mizizi na kuathiri pakubwa sio tu lugha ya Kiswahili bali pia lugha ya Kiingereza kila uchao.

Mbinu mwafaka zikitumiwa tutapiga hatua kubwa katika kuikuza lugha ya Kiswahili hata kuletga usawa katika sekta hii ya elimu katika shule za chekechea. Juhudi hizi zitaweka msingi thabiti wa kukuza na kufuunzia stadi muhimu ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika.

31. Mwanafunzi wa chekechea huweza kuanza shule akiwa na miaka mingapi?
A. Sita
B. Mitatu
C. Saba
D. Minne

32. Mpangilio wa masomo ya kiwango fulani cha elimu huitwa
A. mitara
B. mitaala
C. arudhi
D. ratiba

33. Ni nini maana ya neno chekechea?
A. Hali ya kucheka mwenzako.
B. Shule ya nyuni walao nafaka .
C. Shule ya awali.
D. Kitu kisicho na thamani yoyote.

34. Nomino 'Kiswahili na Kiingereza' ziko katika ngeli ya
A. KI- KI
B. KI- VI
C. KU- KU
D. U-ZI

35. Lugha zote mbili hutumika katika shule za umma zaidi hususan;
A. vyuo vikuu
B. Kiingereza na Kihindi
C. Kisawahili na King'eng'e
D. Kiingereza na Kichina

36. Ni neno lipi ambalo halifai katika orodha ifutayo
A. mpoto
B. lodi
C. tajiri
D. bwenyenye

37. Ni gani si stadi kulingana na kifungu hiki
A. kusikitiza
B. kuchambua
C. kuandika
D. kusoma

38. Ni nini maana ya kiunganishi aghalabu?
A. mwenye mali
B. pindi tu
C. mara nyingi
D. mara kwa mara

39. Lugha ipi ambayo husisitizwa zaidi kwenye shule za kibinafsi
A. lughasimo
B. Kiswahili
C. kichina
D. King'eng'e

40. Ni methali ipi ambayo itafaa maelezo haya "kila mashikadau ahusike"
A. kila mwamba ngoma ngozi huvuta kwake
B. kunguru mwoga hashindwi na mbawaze
C. makataa wengi ni mchwi
D. jungu kuu halikosi ukoko.

***Soma ufahamu ifuatayo kisha ujibu maswali* 41 – 50.**

Alizaliwa takribani miongo miwili katika kitongoji duni cha Matopeni. Kama alivyojulikana Subira alilelewa na wavyele wake wasiokuwa na be wala te. Hali hii ilimpa msukumo wa kuuboresha mustakabali wake pamoja na aila zake kwani damu ni damu si kitarasa.

Pindi tu alipojiunga na shule ya Shaurimoyo, wenzake waliicheka, wakaibeza na kuitemea mate hali yake. Alimeza mrututu na kufululiza moja kwa moja hadi ofisini pa mwalimu wake wa darasa Siti Pendo. Subira alimsimulia yote yaliyojiri dhahiri shahiri. Aidha alimfungulia roho kuihusu aila yake na jamaa zake. Michirizi ya machozi ilipita mashavuni pake kwa dharau kweli ng'ombe wa maskini hazai pacha.

Mintarafu ya hayo, Siti Pendo alikata shauri kumwauni kwa hali na mali. Vilevile aliwahusisha wadarisi wenzake ili kuyakimu barabara matakwa ya Subira. Ama kwa hakika kumpa mwenzako si kutupa.

Kutokana na fadhili na wema aliotendewa, kijana huyu aliuma uzi masomoni. Kila siku alidamka wakati wa majogoo angaa kudurusu na kubukua matopa ya vitabu kwa kutumia taa aina ya koroboi.

Baadaye angeoga kwa maji baridi shadidi mfano barafu. Kiamsha kinywa kwake likawa neno lililotiwa kwenye kamusi kimakosa. Naam! Dau la mnyonge haliendi joshi.

Walipoufanya mtihani wa mwisho wa muhula wa pili, alishika hatamu, akapita kwa shingo na kuibuka nambari ya kwanza. Wadarisi walifurahia matokea yake na kumpa zawadi kochockocho pamoja na wanafunzi wengine walionawiri vyema masomoni. Taibu! chanda chema huvikwa pete.

Baadaye alijiunga na chuo kikuu cha Tumaini alikosomea taaluma ya uhandisi. Alihitimu na shahada hiyo baada ya miaka aruba. Hivyo basi alipata mwaliko wa kampuni moja maarufu jijini Tuletuvune. Hivi leo yeye ni mkurugenzi mkuu wa kampuni iyo hiyo aisee mchumia juania hulia kivulini.

Isitoshe amewajengea wavyele wake nyumba ya kifahari na kuwasomesha wanuna wake wote hadi chuo kikuu cha Kilele. Waambao waliamba kuwa damu ni nzito kuliko maji. Hajawasahau wanakijiji ambao walimfaa kwa hali na mali. Ametafuta mbinu mwafaka angaa kuwatafutia wote wakubwa kwa wadogo.

Hapo ndipo nikabaini ya wahenga kuwa chako ni chako si chetu. Aidha, mgaagaa na upwa hali wali mkavu.

41. Aya ya kwanza inatudokezea kuwa
A. aila ya kina Subira ilikuwa na ulalahoi
B. Subira alikuwa tayatima
C. mhusika hakuwa na nia ya kuisaidia familia yake
D. walimiliki mashangingi kadhaa

42. Ni nini maana ya msemo kumeza mrututu kama. ilivyotumika
A. alimeza dawa chungu
B. alikasirika
C. alijishaua kwa maringo
D. alitafunatafuna mizizi ya miti

43. Ni sifa gani ya Siti Pendo inayojidhihirisha katika aya ya tatu
A. karimu
B. binafsi
C. mtovu
D. mashirikina

44. Tunaweza kusema katika aya ya nne kwamba Subira alikuwa na bidii za ____ ajengaye ______
A. nyuki, mzinga
B. duduvule, gongo
C. nyuki, kichunguu
D. mchwa, kingulima

45. Fadhili na wema ni aina ya nomino gani
A. kawaida
B. dhahania
C. jumla
D. makundi

46. Tunaambiwa kuwa Subira alishika hatamu , ina maana kuwa
A. aliongoza darasa kama kiranja
B. alilemewa na masomo
C. alipata maradhi na kulazwa hospitalini
D. wenzake darasani walimtazama kisogoni

47. Ni nini maana ya uhandisi
A. taaluma ya uwekaji hesabu za kampuni
B. kutibu magonjwa sugu hopsitalini
C . fundi wa mitambo
D. kubeba bidhaa mgongoni , kichwani na begani

48. Maneno kama vile Tumaini, Subira, Pendo Tuletuvune, Matopeni .. yametumia mbinu ipi ya uandishi
A. tashdidi
B. majazi
C. tashhisi
D. taharuki

49. Ni neno gani ambalo halifai katika orodha hii
A. kiamshakinywa
B. kisebeho
C. staftahi
D. kilalio

50. Teua mada mwafaka ya hadithi uliosoma
A. Dau la mnyonge haliendi joshi.
B. Kikulacho ki nguoni mwako.
C. Kichwa cha kuku hakistahimili kilemba.
D. Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.